




Mbuni na Simba
walikuwa marafiki
sana. Wote wawili
walikuwa na
watoto wachanga.



Mbuni aliwalisha
watoto wake vizuri.



Watoto wa Simba
hawakupata
chakula cha kutosha.



Simba aliwaangalia
vifaranga nakuwaza,
"Hawa ni wazuri!
Natamani wangekuwa
wangu!"



Wakati Mbuni
alikuwa hayupo,
Simba aliwachukua
watoto wa Mbuni
akaenda nao
nyumbani kwake.



Mbuni alirudi na
kupata watoto wa
Simba nyumbani
kwake. Alilia,
"Watoto wangu
wako wapi?"



Mbuni alikimbia nyumbani kwa Simba. Aliwapata wanawe wakiwa na Simba.




Simba alikataa
kuwarudisha
watoto wa Mbuni.
Alisema, "Hawa ni
wangu sasa.
Unaweza
kuwachukua
watoto wa simba."




Mbuni alikasirika sana. "Nitafanyaje ili niwapate watoto wangu?" Alijiwazia.



Halafu alifikiri,
"Ninajua
nitakachokifanya.
Nitawaita
wanyama wote
kwa mkuano."



Wanyama
walikubali
kukutana.



Tembo aliwaauliza
Mbuni na Simba
kuzungumza.



Wanyama wengi
waliogopa
kumlaumu Simba.



Mwishowe, Kuchakuro
alisimama na kusema,
"Watoto ambao
wanafanana na ndege
ni wa Mbuni. Watoto
ambao wana mikia ni
wa Simba jike."



Kuchakuro
alitorokea tunduni.
Wanyama wote
walishangilia.



Simba alikasirika
sana. Alienda
nyumbani na
watoto wake.